**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**650** **HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2019**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Toa hoja nne kuonesha uhusiano uliopo kati ya kitabu cha kiongozi cha mwalimu na muhtasari wa somo.
2. Changanua mambo makuu manne ambayo mwalimu anatakiwa kuyafikiria kabla ya kuanza kufaragua na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.
3. Toa hoja nne kwa kueleza kwa kifupi sababu za kufanya uchambuzi wa kiongozi cha mwalimu katika kufanya maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
4. Fafanua kwa kifupi aina nne za maswali yanazoweza kutumika kupima maendeleo ya wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
5. Toa maana ya dhana nne kama zinavyotumika katika somo la Haiba na Michezo:
   (a) Kufaragua
   (b) Zana za kufundishia na kujifunzia
   (c) Zana mpitisho
   (d) Zana mafunzo
6. Eleza kwa kifupi maana ya istilahi:
   (a) Ujuzi
   (b) Lengo kuu
   (c) Mada ndogo
   (d) Lengo mahsusi kama zinavyotumika katika uandaaji wa andalio la somo la Haiba na Michezo.
7. Toa hoja nne kuonesha uhusiano uliopo kati ya azimio la kazi na andalio la somo.
8. Ainisha pasi nne za msingi ambazo mwanafunzi anatakiwa kujifunza ili kumwezesha kucheza mpira wa kikapu kwa ufanisi.
9. Bainisha mada nne zinazoweza kufundishwa kwa kutumia msingi unaolenga ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya vitendo.
10. Pendekeza njia nne zinazoweza kutumika kubadilisha wanafunzi wenye tabia zisizofaa na kuwa na tabia zinazokubalika.

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Tumia hoja tano kueleza vipengele vya sehemu ya maudhui katika muhtasari wa somo ambavyo humsaidia mwalimu katika maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji.
12. Changanua zana tano zinazoweza kutumika kufanya tathmini ya ujifunzaji wa wanafunzi katika nyanja mbalimbali katika somo la Haiba na Michezo.
13. Eleza kwa hoja tano kuhusu vyanzo vinavyoweza kumsaidia mwalimu wa somo la Haiba na Michezo katika kuandaa tini za kufundishia na kujifunzia.
14. Fafanua misingi mitano ambayo mwalimu anapaswa kuzingatia wakati wa utungaji wa maswali ya kweli au si kweli.
15. Toa tathmini ya namna ambavyo changamoto wanazokumbana nazo watoto wanaoishi katika mazingira duni zinavyoweza kuchangia kuwa na mahudhurio duni shuleni kwa kutoa hoja tano.
16. Fafanua kwa hoja tano umuhimu wa kubainisha idadi ya wanafunzi walioandikishwa na waliohudhuria katika andalio la somo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org